**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Tano – Tarehe 14 Septemba, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera na Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Taarifa ya Serikali kuhusu suala la ukodishwaji wa nyumba inayotumika kwa ajili ya vipimo vya Covid 19 Mazizini.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Taarifa ya Serikali kuhusu suala la ukodishwaji wa nyumba inayotumika kwa ajili ya vipimo vya Covid 19 Mazizini.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

52. MHESHIMIWA MOH'D MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Kwa nia njema kabisa, Baraza la Wawakilishi Zanzibar lilipitisha Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Matukio ya Kijamii kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii zikiwemo vyeti vya kuzaliwa, ndoa na talaka. Huduma zote hizo zinatolewa chini ya usimamizi wa Mkuu wa Kituo cha Usajili.

    (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuyaimarisha maslahi ya wakuu wa vituo hivyo, hasa ukizingatia maslahi yao ni madogo yasiyolingana na majukumu makubwa ya kitaifa waliyokabidhiwa.

    (b) Ni lini Serikali itawapatia usafiri wakuu hao utakaowawezesha kufuatilia utekelezaji wa majukumu yao wanapohitaji kwenda Makao Makuu ya Afisi yao.

### Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

65. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

    Zanzibar ilikuwa na idadi kubwa ya viwanja vya michezo, vipo vya Wilaya, Skuli na maeneo mbali mbali mfano Mnazi Mmoja na Tumbaku.

    (a) Je, Serikali inafahamu kuwa viwanja vingi sasa vimevamiwa na baadhi ya maeneo wananchi wanakosa sehemu za kucheza michezo mbali mbali.

    (b) Kwa kuwa baadhi ya maeneo ya viwanja yanatumiwa kwa shughuli nyengine. Je, timu zilizokuwa zikitumia viwanja hivyo zimezingatiwa.

    (c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza maeneo ya viwanja.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

134. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali imekuwa ikitoa miongozo mizuri kuhusu vigezo vya ajira kwenye taasisi za umma nchini. Hata hivyo, ajira nyingi hazikuwa zikizingatia zaidi elimu na kutovipa umuhimu mkubwa wa kiwango cha ujuzi na uzoefu.

(a) Je, ni upi mpango wa Serikali katika kuwianisha elimu, ujuzi na uzoefu kuelekea uchumi wa buluu.

(b) Je, Serikali imejiandaaje kupata wataalamu wenye uwiano wa elimu, ujuzi na uzoefu katika viwanda sambamba na uchumi wa buluu.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

117. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda.

Serikali inastahili pongezi kwa jitihada zake za kulienzi zao la karafuu. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko mengi katika msimu huu wa mwaka 2021 kuhusiana na vigezo na utambuzi halali wa daraja (grades) zake anazopatiwa mkulima na Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC) kwa niaba ya Serikali na zaidi katika ulazima wa kutumia njia ya elektroniki katika malipo.

(a) Je, ni njia gani za uhakika na usawa hutumika katika kutambua vigezo na utambuzi halali wa daraja (grades) za karafuu.

(b) Ili kuondoa malalamiko, Je, Serikali haioni ipo haja ya kutumia mifumo ya kompyuta na elektroniki katika kutambua vigezo vya daraja halali za karafuu.

(c) Je, mchakato upi uliotumika katika kuamua matumizi ya elektroniki katika malipo ya mauzo ya karafuu kwa wakulima wadogo upigaji marufuku uokotaji wa mpeta kwa mwaka huu kinyume na ustaarabu uliozoeleka.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

146. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa kuwa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ina tatizo la upotevu wa maji unaosababishwa na uvujaji wa mabomba.

(a) Je, Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) wanacho kifaa cha utambuzi wa uvujaji wa mabomba.

(b) Endapo Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) wanacho kifaa hicho, Je, miundombinu yetu ya maji ni rafiki kuweza kufanikisha kifaa hicho kufanya kazi.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

20. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kwa kuwa wakaazi wa Jimbo la Kojani hutegemea zao la mpunga kwa ajili ya chakula, na kwa kuwa katika msimu huu wa kilimo zao hilo limeathirika sana kutokana na uhaba wa mvua, jambo ambalo limewaweka wananchi wa Kojani pamoja na maeneo mengine katika hali ngumu ya kimaisha. Na kwa kuwa Serikali za awamu zilizopita zilikuwa na utaratibu wa kuwasaidia wakulima wanapopatwa na janga kama hili.

Je, ni lini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itatoa msaada wa kibinaadamu kwa wakulima hawa ili kuwapunguzia ugumu wa maisha.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

102. MHESHIMIWA HUDHAIMA MBARAK TAHIR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Miongoni mwa malengo ya Sera ya Utalii ni kubadilisha aina ya utalii tulionao zaidi hivi sasa wa vishuka na kuelekea katika utalii unaoleta tija kubwa (High End Tourism) ambapo tunatarajia kupata watalii wa kipato cha juu.

(a) Je, Wizara imefikia hatua gani katika kuitekeleza sera hii ukilinganisha na vikwazo vilivyoikabili dunia.

(b) Je, Wizara imechukua hatua gani za dharura katika kulinda uchumi wetu unaotokana na utalii.

(c) Je, Wizara imenufaisha vipi vijana wa Zanzibar katika utalii baada ya mabadiliko ya Sera ya Utalii yaliyofanyika kwa mara ya mwisho.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

12. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Wizara yako imekuwa ikilalamikiwa sana katika suala la ulipaji wa fidia kisiwani Pemba wakati inapojenga barabara. Kadhia hii pia imewakuta wananchi wa jimbo la Micheweni hasa katika maeneo ya uchimbaji wa kifusi.

(a) Je, kiasi gani cha fedha kinachodaiwa na wananchi wa kijiji cha Maziwa Ng’ombe, waliotoa ushirikiano kutoa mashamba yao kwa kupisha ujenzi wa barabara inayotoka Micheweni kuelekea maeneo ya uwekezaji.

(b) Ni lini fedha hizo zitalipwa kwa wananchi wa kipato cha chini, ili watafute mbadala wa kianzio chengine cha kujipatia riziki.

(c) Ni lini Serikali itakuwa na mkakati wenye uhakika wa kutathmini athari na makisio halisi kabla ya utekelezaji wa miradi ili ilipe fidia za wananchi kwa wakati.

16. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika miezi ya hivi karibuni kumekuwa na malalamiko ya wasafiri wa boti hasa katika bandari ya Dar-es-Salaam kuwa boti hizo haziondoki kwa wakati uliopangwa hali inayopelekea kuvuruga ratiba ya shughuli zao na kuwatia hasara kiuchumi.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha safari za boti zinaenda sambamba na ratiba halisi.

(b) Kuna mashirikiano gani kati ya Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) na Mamlaka ya Bandari (TPA) katika kukabiliana na tatizo hilo.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

87. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali ya Awamu ya Nane imejipambanua kuinua uchumi wake kupitia uchumi wa buluu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwainua kiuchumi wananchi wa jimbo la Wawi hususan vijiji vya Kibokoni, Furaha na Mvumoni kupitia uchumi wa buluu.

92. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Katika kuimarisha uvuvi hapa nchini, Serikali ilituahidi sisi wananchi wake kuwa, itanunua meli za kisasa za uvuvi wa bahari kuu, lakini ahadi hiyo hatimae imetekelezwa kwa kununuliwa maboti, badala ya meli hizo za kisasa za uvuvi.

(a) Je, Serikali imetumia gharama ya kiasi gani kwa ununuzi wa boti hizo.

(b) Je, Serikali inapata faida na hasara ya kiasi gani katika ununuzi wa maboti ya uvuvi hapa nchini.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

17. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Kwa kuwa wananchi wa kisiwa cha Kojani katika Jimbo la Kojani tayari wanacho Kituo cha Afya. Na kwa kuwa daktari aliyekuwepo katika kituo hicho ni mmoja ambaye hakidhi haja

ukilinganisha na idadi ya wakaazi wa kisiwa hicho, na kwa kuwa daktari huyo hulazimika siku nyengine kufanyakazi nje ya kisiwa hicho huku wananchi wakikosa huduma muhimu ya afya.

Je, ni lini Wizara itaajiri daktari mkaazi wa kisiwa hicho ili kuondosha adha inayowapata wakaazi wa Kojani, ukitilia maanani tayari wapo vijana ambao wameshasomea fani ya Afisa utabibu (Clinical Officer).

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

105. MHESHIMIWA SAADA RAMADHAN MWENDWA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja, Serikali kupitia Wizara hii imekuwa ikifanya ukarabati wa nyumba nambari moja (1) katika eneo la Michenzani kwa kupaka rangi. Hata hivyo, ujenzi huo unaenda pole pole sana.

(a) Je, Wizara imeridhia ukarabati huo na utachukua muda gani hadi kukamilika kwake.

(b) Je, mpaka kufikia hatua hiyo, ni kiasi gani cha gharama kilichotumika hadi sasa katika ukarabati huo.

## III. TAARIFA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera na Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Taarifa ya Serikali kuhusu suala la ukodishwaji wa nyumba inayotumika kwa ajili ya vipimo vya Covid 19 Mazizini.

**Zanzibar,**
**14 Septemba, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**